

HALMSHAURI YA WILAYA YA NGARA
MUHTASARI NAMBA 6 WA KIKAO CHA KAMATI YA WATALAAM CMT
KILICHOFANYIKA TAREHE 14/12/2021

WALIOHUDHURIA:

1. Bw. Solomon O. Kimilike - Mkurugenzi Mtendaji- Mwenyekiti
2. Bw. Richard Sentoce -Kaimu Mkuu wa Idara Utawala na Utumishi -Katibu
3. Bw. Didmus Bamuhiga - Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
4. Bw. Remigius Kawishe - Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
5. Bw. Ezra Sasage -Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
6. Bw. Simon Mtuka -Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto
7. Bw. Patrick Ogo - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
8. Bi. Elionora William - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
9. Bi. Asante Karara - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
10. Bw. Gwassa Kadende - Kaimu Afisa Maliasili
11. Bi Jusline Bandiko - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
12. Bi Perpetua Lutwaza -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
13. Bw. Victor J. Bachukwita - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
14. Bw. Zacharia Mkumbo - Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari
15. Bi. Irene Mwakabanga -Kaimu Afisa Biashara
16. Bi Sakina Y. Chamiti - Mratibu wa TASAF
17. Emmanuel Victor - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
18. Bw. Cosmas Rubambura - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi

Sekretarieti

1. Bi. Reinfrida Anzigary - Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri
2. Bi. Vivian Maruhe - Mwandishi wa Vikao

AGENDA NA. 21/MUHT NA 6/12/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwasalimia wajumbe na kumkaribisha Mwenyekiti aweze kufungua kikao. Mwenyekiti aliwasalimia wajumbe na kuwakaribisha. Kikao kilifunguliwa saa 2.28 asubuhi.

AGENDA NA. 22/MUHT NA 6/12/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA

Wajumbe walipitia agenda na kuridhia zianze kujadiliwa

AGENDA NA. 23/MUHT NA 6/12/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

Wajumbe walipitia muhtasari na kufanya masahihisho. Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliridhia Katibu na Mwenyekiti kuweka saini zao ili uwe kumbukumbu halali za kikao.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili kama ifuatavyo;

Ilisisitizwa kwamba mwongozo wa ujenzi uambatanishwe katika taarifa itakayowasilishwa katika kikao cha fedha utawala na mipango

Ilihojiwa kwamba ni kwanini yabomolewe majengo matafu tu nay a siwe majengo mengine na kujibiwa kwamba mwongozo unaelekeza kwamba jengo lijengwe karibu na chumba cha upasuaji na liwe mbele.

AGENDA NA. 29/MUHT NA 6/12/2021/2022: TAARIFA INAYOHUSU UJENZI WA JENGO LA HUDUMA ZA DHARURA (EMD) NA NYUMBA YA WATUMISHI 3/1 ITAKAYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA UVIKO-19

Iliwasilishwa kwamba Idara ya Ujenzi na Afya zilishiriki semina elekezi iliyofanyika Dodoma kuanzia tarehe 2-3/12/2021, semina ilitolewa na Ofis ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo Jinsia , Wazee na Watoto na Taasisi ya "Abbott Fund Tanzania".

Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tshs. 390,000.00 kwa mchanganuo ufuatao;

- i. Jengo la magonjwa wa dharura Tshs. 300,000,000
- ii. Nyumba ya watumishi 3/1 Tshs. 90,000,000

Maelekezo yaliyotolewa ni pamoja na;

- I. Utaratibu wa ujenzi utakaotumika ni wa kutumia wakandarasi daraja la kwanza hadi la nne tu kutokana na uhitaji wa utaalum maalum
- II. Lazima Mkandarasi aoneshe mpango kazi wake
- III. Mpangilio wa jengo la Idara ya magonjwa ya dharura izingatie ukaribu na majengo ya OPD na jengo la upasuaji
- IV. Mwezi Desemba, 2021 taratibu zote za manunuzi ziwe zimekamilika
- V. Tarehe 4 mwezi Januari ujenzi uanze mara moja bila kuchelewa
- VI. Mradi utatekelezwa kwa muda wa miezi 4 na tarehe 30/4/2022 ndiyo siku ya kukabidhi mradi
- VII. Hakutakuwa na ongezeko la muda wa utekelezaji wa mradi
- VIII. Eneo la utekelezaji wa mradi ni Hospitali ya Nyamiaga na majengo yatakayoathirika ni
 - a. Jengo la OPD
 - b. Jengo la Bima

c. Na baadhi ya njia za kwenda mawodini

Wajumbe waliipokea taarifa na kuipitisha.

**AGENDA NA. 30/MUHT NA 6/12/2021/2022: MENGINEYO
MADENI YALIYOZALISHWA KATIKA MRADI WA WASH**

Ilihojiwa kuwa katika kuhakiki madeni hayo kuna vielelezo vyovyote vinavyoonesha au kuthibitisha uhalali wa madeni hayo.

Mwenyekiti alisisitiza kwamba maelekezo aliyoyatoa juu ya madeni ya vyoo vya WASH yafanyiwe kazi mara moja baada ya kukamilika wajumbe wa kamati ya CMT wapatiwe taarifa

AGENDA NA. 31/MUHT NA 6/12/2021/2022: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kikao kilifungwa rasmi saa 7.46 mchana.



.....
Katibu

UMETHIBITISHWA NA:



.....
Mwenyekiti

Tarahahe.....09/02...../2022